



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA LUSHOTO



MKOA WA TANGA:
SimuNa:027-2977216
Telefax:027-2977217
E-mail:ded@lushotodc.go.tz
Website:www.lushotodc.go.tz
Ukijibu tafadhali nukuu:
Kumb.Na.LDC/C.20/19/93

18 Barabara ya Halmashauri
S.L.P. 32,
21782 Lushoto,Tanga.

Tarehe 16/09/2023.

Wananchi wote,
TANZANIA.

TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto anawatangazia waombaji wote walioomba nafasi za kazi za Katibu Mahsusi Daraja la II na Mtendaji wa Kijiji Daraja la III kutokana na Tangazo la kazi Kumb.Na.LDC/20/19/82 la tarehe 20/06/2023 kuwa wafuatao wamechaguliwa kufika kwenye usaili.

Usaili huo utafanyika kama inavyoonekana kwenye Jedwali lifuatalo:-

RATIBA YA USAILI

| NA | KADA | TAREHE YA USAILI WA MCHUJO | TAREHE YA USAILI WA VITENDO | TAREHE YA USAILI WA MAHOJIANO | MAHALI |
|----|----------------------------------|----------------------------|-----------------------------|-------------------------------|-----------------------------------------------------|
| 1 | Katibu Mahsusi Daraja la II | Hakuna | 21-09- 2023 | 22- 09 - 2023 | Ukumbi wa Halmashauri |
| 2 | Mtendaji wa Kijiji Daraja la III | 23-09-2023 | Hakuna | 24 na 25- 09- 2023 | Kumbi za Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) |

Masharti ya Ujumla:-

- Wasailiwa wanatakiwa kufika na vyeti halisi vya Kidato cha IV/VI,Taaluma na kuzaliwa.

- b) Wasailiwa waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na mamlaka husika (NECTA na NACTE).
- c) Wasailiwa watajigharamia wenyewe usafiri, malazi na chakula.
- d) Wasailiwa wanatakiwa kufika katika ukumbi wa usaili saa 2.00 asubuhi.
- e) Kila msailiwa anatakiwa kufika na mojawapo ya vitambulisho vifuatavyo kwa ajili ya utambuzi. Vitambulisho hivyo ni:- kitambulisho cha NIDA, kitambulisho cha mpiga kura, kitambulisho cha mkazi, hati ya kusafiria, leseni ya gari na barua ya utambulisho toka serikali ya kijiji au mtaa.
- f) Waombaji wote ambao majina yao hayajaonekana kwenye orodha iliyoambatishwa watambue kwamba hawakukidhi vigezo hitajika.

Imetolewa na Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto.


.....
Ikupa Harrison Mwasyoge
Mkurugenzi Mtendaji (W)
LUSHOTO